# *SANATAN DHARM*

(Dhehebu la dini ya Kibaniani)

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

# SANATAN DHARM

(Dhehebu la dini ya Kibaniani)

Tafsiri ya Kiswahili ya: Sanatan Dharm (Kiurdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri: Sheikh Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1903
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): Tanzania, Kenya 2016

© Islam International Publications Ltd.

Kwa maelezo zaidi:
**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744
**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania – Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-544-6

ٹائیٹل بار اول

چونکہ اس رسالہ میں انصاف کی رو سے کسی قدر

سناتن دھرم کی مدد ہے اس لئے

اس کا نام

# سناتن دھرم

رکھا گیا

تصنیف لطیف حضرت مسیح موعود و مہدی مسعود امام الوقت

علیہ السلام میرزا غلام احمد صاحب قادیانی سلمہ اللہ الرحمان

۸ مارچ ۱۹۰۳ء

مطبع ضیاء الاسلام قادیان دار الامان میں باہتمام حافظ

حکیم فضل الدین صاحب کے چھپ کر شائع ہوا

تعداد اشاعت ۲۰۰۰

بار اول

Jalada la chapa ya mara ya kwanza

Kwa vile ndani ya kijitabu hiki dhehebu la Sanatan Dharm limesaidiwa kiuadilifu kiasi fulani, hivyo kimeitwa jina

# SANATAN DHARM

Uandishi murua wa Hadhrat Masihi Mau'udi na Mahdi Mtukufu, Imam wa zama, Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, Mungu Mrehemevu Amweke salama.

8 Machi 1903

Kimechapishwa katika kiwanda cha uchapaji cha Dhiaul Islam Qadian, Darul-Amaan,

chini ya usimamizi wa

Bwana Hafidh Hakim Fadhluddin na kuenezwa.

Idadi ya nakala: 2000 Chapa ya mara ya kwanza

## Neno La Mfasiri

Nafurahi kuweka mbele ya wasomaji tafisiri ya Kiswahili ya kitabu kingine tena cha Seyidna Ahmad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Kitabu chenyewe chaitwa Sanatan Dharm.

Sanatan Dharm ni dhehebu mojawapo la dini ya Kibaniani. Wafuasi wa dhehebu hili wanaamini kwamba Mungu ni mwumbaji wa vitu vyote, lakini Ameyajaalia masanamu uwezo mwingi sana. Hivyo, wanayaabudu masanamu na kuyaomba msaada wakiamini kuwa yanawasaidia katika mambo yao.

Katika kitabu hiki mtakuta pia habari za dhehebu jingine la Kibaniani liitwalo Aria Samaj. Hao wanakataa katakata ibada ya masanamu, lakini ubaya wao ndio mafundisho mawili.

La kwanza, wanaamimi kuwa roho na mata vipo tangu azali, havikuumbwa na Mungu. Mungu si mwumbaji wa kitu chochote, bali kazi yake hasa ni kufanyiza wanadamu, wanyama na vinginevyo kwa kutumia hiyo 'mali ghafi' — roho na mata.

La pili laitwa *Neyoga*. Neno hili la lugha ya Kibaniani tafsiri yake ni ruhusa, amri. Katika

istilahi yao *Neyoga* yamaanisha kumhalalishia mke asiyemzalia mumewe mtoto ama mtoto wa kiume kwamba yuaweza kulala na ndugu wa mumewe au mtu yeyote mwingine ili kumzalia mumewe mwana. Yaani, mzaliwa atanasibiwa kwa mume wa huyo mke mwenye bahati mbaya sio kwa mtu aliyemwingilia. Na kwa njia ya *Neyoga* mama huyo anaruhusiwa kazaa wana hadi kumi na mmoja. Katika kitabu hiki madhehebu yote mawili yametolewa nasaha ya kujirekebisha.

Hatimaye njia tatu za kuchunguza ukweli wa dini zimeelezwa kinagaubaga.

Nawatolea shukurani Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Mbashiri Mkuu wa zamani katika Tanzania, aliyekisoma kwa uangalifu kabla hakijapigwa chapa, na Sheikh Ansar Hussain aliyepanga maandishi haya kwa kompyuta, na pia Seyid Tanwir Mujtaba aliyefanya kazi ya *fometi*. Mwenyezi Mungu Awapatie wote hao malipo bora. Amin.

Jamil R. Rafiq

Wakilut Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan
18 Januari 2016

## Tafsiri ya Shairi alilotunga mwandishi.

Enyi Wa-Ariya Samaj,[1] msijinase ndani ya adhabu. Enyi marafiki! mbona mmepatwa na mawazo mabaya?

Ewe kaumu ya Aria, moyo wako umekuwaje? U macho, ama waongea usingizini?

Je yule Aliye Mungu siye Mungu wa roho yako? Hamna hata alama ya imani ndani ya jibu lako kama hilo.

Kama roho ya wampendao haitokani na Mkono Wake, kwa nini hawanao utulivu kwa wengine.

Kama Ametengana kabisa hata kwamba Hajaigusa roho, yu nani tena aliyetia mapenzi Yake moyoni?

Jinsi zichomwavyo nyoyo za wampendao Yeye, hatujauona mchomo kiasi hicho hata katika kababu.

Afaye hupatiwa ukaribu Wake, hapo hamna tofauti baina ya mzee na kijana.

Ajifiaye Kwake ndiye ampataye Yeye; hapo maneno matupu hayana maana.

---

[1] Aria Samaji ni dhehebu moja la dini ya Kibaniani mbali na dhehebu la Sanatan Dharm. — Mwenezi.

Yeye Huwa wa yule aliyekuwa Wake, yu mapajani Mwake aliyeangukia Kwake.

Nenda ukaone maua, mng’aro wake hutokea Kwake, nuru Yake hung’ara katika mwezi na jua.[2]

Katika uzuri wa wazuri pia kuna nuru Yake. Ni kitu gani uzuri? Ni Yeye tu Aliyemulika nyuma ya pazia.

Kila unywele wa shungi huelekeza Kwake, huwa katika wayowayo kwa kukaa mbali Naye.

Tazameni, kila jicho la kuvutia lamwonyesha Yeye; kila fuadi hupata kuungua katika penzi lake.

Majahili wasioyakinia mambo Yake wanatafuta maji mazigazini.

Waukataa uwezo wa Yule Mweza, hupayuka kama yule aliyelewa chakari.

Hawanayo moyoni hamu ya kumwona Yule Mtukufu, huwaogopa watu isije wakawashika katika hasira.

Ee Azizi, tuonyeshe sisi ile jamali yako, mpaka lini Uso ule utabaki mafichoni nyuma ya pazia!

---

[2] اَللّٰهُ نُوْرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ Mwenyezi Mungu ni nuru ya mbingu na ardhi. (aya ya Kurani Tukufu) An Nur, 24:36 — Mwenezi.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ[3]

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ[4]

## NEYOGA

Ingawaje katika kitabu cha ‘Nasim-e-Da‘wat’ nimekwisha zungumzia *Neyoga* ipasavyo, nami naelewa kuwa hayo yamfaa na kumtosheleza sana atafutaye haki, lakini nimewahi kuwasikia baadhi ya watu wakisema kwamba Pandit Ram Bhajdat, Raisi wa Baraza la Aria la Panjab, baada ya kupokea kitabu changu Nasim-e-Da‘wat akasema akinizungumzia katika mkutano wa Aria Samaji mjini Qadian katika hotuba yake ya mwisho kwamba “Kama yeye angeongea nami juu ya *Neyoga*, ningemweleza faida zake zote.”

Hivyo, kwa adabu nasema kwamba kadri itakikanavyo kwa ghera ya mtu na dhamiri safi ya binadamu nilieleza kwa nia njema ndani ya kitabu changu Nasim-e-Da‘wat. Shabaha yangu haikuwa

---

[3] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu — Mwenezi.

[4] Twamhimidia yeye na twamsalia Mtume wake Mtukufu. — Mwenezi.

kufanya mjadala; hiyo ilikuwa ni nasaha tu kwa njia ya huruma. Nami sipo peke yangu katika jambo hili, maelfu ya Mabaniani waungwana, na Masingasinga waungwana washikamanao barabara na dini ya Kisingasinga, hawahalalishi jambo hili kwamba mwanamke mwenye mume na wa ukoo wenye heshima aingiliwe na mwingine ilhali mumewe yupo hai, kwa tamaa tu ya kupata watoto.

Hizo faida za *Neyoga*, pengine bwana Pandit anamaanisha ni faida za kupata watoto wa *Neyoga*, yaani watoto kumi na mmoja wanapata kuzaliwa bure, na hivyo idadi ya wazao huzidi. Lakini bwana Pandit asikasirike kuambiwa kwamba wazao kama hao ndio doa baya kwa mtu mwungwana, siyo sababu ya fahari. Kwa rai yangu, mwanamke mwema kama akiishi maisha mazima bila kuzaa, basi afadhali kufa bila kupata watoto kuliko kulalana na mtu mwingine na kuzaa watoto ambao kiakili waitwe kuwa ni wa haramu. Na kama kipo kitu kiitwacho ukweli, basi kwa nini watoto hao wanasibishwe kwa huyo mume mwenye bahati mbaya ambaye mkewe akazini na watoto sio kwa shahawa yake; bali hao ndio wazao wa wale ambao kwa shahawa yao wametokana. Laiti mwanamke kama huyo

angekufa kabla hajapata watoto kama hao, hiyo ingekuwa afadhali. Haifai kwa Pandit Ram Bhajdat kung’ang’ania sana suala la aibu la *Neyoga*. Bali kwa kuwa suala hilo ni kinyume cha staha ya mtu, hivyo yafaa liondolewe mbali katika mafundisho ya Aria Samaj na itangazwe hadharani kuwa Dayanand akafanya kosa kubwa kwa sababu ya kukaa kapera maisha mazima na kutokuhisi ile ghera aliyo nayo kila mume mwungwana katika hali ya maisha ya ndoa kumhusu mkewe, kwa hiyo Aria Samaj inaiondolea mbali hiyo kutoka katika mafundisho yake. Tangazo hilo lapaswa lisainiwe na watu wengi ili mkinzani yeyote asipate tena nafasi ya kupinga. La sivyo, wakumbuke kwamba fundisho la *Neyoga* ni ndwele kwa dini yao. Nami siwezi kukubali kwamba wanawake wenye staha watakuwa tayari kwa kufanyiwa *Neyoga*, bali nahofia isije mwanamke yeyote akajiua kwa kula sumu akikazaniwa kutenda kitendo hicho.[5] Enyi mabwana, kilichokwisha fanyika kimefanyika,

[5] Hadi sasa kinamama wa India wamekuwa na uhusiano wa kweli na waume zao hata kwamba wakajitupa kimbwini mwa kuchomea maiti za waume zao. Lakini yule mwanamke aliye na mumewe na analalana na wengine, anawezaje kuwa na upendo kwa mumewe? — Mwandishi.

lakini liondoleeni balaa hili katika kaumu yenu haraka, na msilinasibishe kwa Veda. Msitarajie kuwa wanaume waungwana na wanawake waungwane wa nchi ya Aria (India) wataikubali, bali nafikiria kuwa desturi ya kupanga mwana nayo imetokana na desturi ya *Neyoga*. Ndiyo kusema kwamba wanaume waungwana na wanawake waungwana walipoona kuwa hiyo ndiyo desturi chafu basi wakaanzisha desturi ya kupangu mwana. Uungwana wa wanaume haukuonelea kwamba waijirishe desturi hiyo chafu, yaani *Neyoga* kwa wake zao, hivyo wakapenda desturi ya kupanga mwana. Ingawaje kupanga mwana ni kitu kilicho feki, lakini hata hivyo ni afadhali kuliko ile desturi pujufu na chafu. Hiyo ni desturi chafu kiasi hiki kwamba hata kama mtu dhalili asiye na hulka njema akishauriwa wakeze wafanyiwe *Neyoga*, huyo atakuwa tayari kupigana hata kuuana. Basi, kwa nini tusiwasikitikie Waaria kwani wakakubali maneno ya Dayanand wakifumba macho. Hao wafuasi wa Sanatan Dharm nao walikuwa ni ndugu zao kidini, je hao walikuwa hawaisomi Veda tangu kale? Mbona hawaipendi desturi hiyo chafu! Nasikitika kwamba kwa kuwahurumia wakiambiwa Waaria hao waachane na desturi

hiyo na wasiwafanye wake zao kutende mambo hayo, huwa wanakasirika. Hali ya wafuasi wa Aria Samaj ni ya ajabu, hawaoni haya hata kidogo. Siku za nyuma niliwakaribisha Waaria wachache nyumbani kwangu, Mwaria mmojawapo akiwa Kishan Singh ambaye amekuwa Mwaria kwa kuchukia kuwa mfuasi wa Bava Nanak — akatengana na mtu aliyekuwa ametukuka na kutakasika naye alikuwa amejaa moyo wake mapenzi ya Mungu, na kumtaja-taja Pandit Dayanand kama uradi. Pamoja naye walikuwa pia Lala Sharampat na Lala Malavamal na Pandit Somraj, katibu wa Aria Samaj ya Qadian na Mabaniani kadha wa dhehebu la Sanatan Dharm. Tukawasihi sana kwamba haifai kuwafanya wake zenu kutendewa mambo kama hayo husuan katika kijiji hiki. Wakati huo wote wakanyamaa nao wakaona haya, lakini Pandit Somraj akasema kuwa hamna ubaya katika kitendo hicho. Hapo wale wafuasi wa Sanatan Dharm waliokuwepo waliposikia kuwa mtu huyo ndani ya kikao kizima akamhalalishia mkewe kitendo hicho kichafu pasipo kuona haya mara wakaanza kutamka Ram! Ram!! (Do masalele!) Na Waaria wengine wakificha nyuso zao katika shuka zao wakaanza kucheka. Pengine watu

karibu thelathini wakamshuhudia yule Pandit alipotamka midomoni mwake neno hilo la aibu.

Nasikitika sana kwamba Waaria hawaiondoi desturi hiyo, bali kwa hamaki wanasema, je Waislamu hawafanyi mut'ah,[6] yaani mwawataliki wanawake walioolewa. Walifahamishwa sana kwamba enye mabwana, wapi talaka inayotolewa duniani kote wakati wa shida na wapi kitendo hiki kwamba mume aliye hai amwamrisha mkewe kuingiliwa na mwingine! Lakini, hao watu hawaifahamu hiyo. Wafuasi wa Sanatan Dharm walio wenye staha na ghera wanakuwa hoi kwa aibu na fedheha — dhambi ya wale, fedheha kwa hao. Waliambiwa mara kwa mara kwamba mtu baada ya kuoa akimtaliki mkewe au akaweka mapema muda maalum kwa kutaliki kwamba baada ya muda fulani atatoa talaka — ambayo baadhi ya Washia wanaiita Mut'ah — ndoa hiyo hailingani na ile desturi yenu. Na ndoa ambayo inawekewa muda fulani wa kutaliki imekatazwa katika dini yetu. Kurani Tukufu inaikataza waziwazi kabisa. Kabla haijafika Islam, Waarabu kwa muda fulani walikuwa na desturi ya ndoa

[6] Mut'ah ndiyo ndoa ya muda. Baadhi ya Washia wanaihalalisha, sio Waislamu wengine. — Mwenezi.

kama hizo, Kurani Tukufu ikazikataza. Kurani Tukufu iliposhuka, hizo zikawa mwiko. Baadhi ya madhehebu ya Washia wanashikamana nayo, lakini hao wamenaswa katika desturi ya kabla ya Islam. Haijuzu kwa mwenye busara kutaja kosa la mwingine ili kusitiri kosa lake mwenyewe. Je, mwenye hatia anaweza kuachiliwa kwa kutaja hatia ya mwingine? Katika Neno la Mungu kuna mwongozo bayana, hamna humo hata habari ya ndoa kama hii ambayo wakati wa kuifunga ielezwe nitatoa talaka baada ya muda fulani. Isitoshe, ukinzani wenyewe kwa hakika ni dhidi ya talaka. Na hakuna kundi lolote duniani liipingalo talaka. Kwa sababu hii au ile pengine talaka huwa haina budi kutolewa. Ilmuradi, Waaria wanapokatazwa wasifanye kitendo cha aibu, hufedheheka na kujibu kwamba Waislamu nao wantoa talaka. Enye mabwana, katika dini ipi desturi hii haipo? Mume na mke wanapokosana vikali itakuwa njia gani ya kusalimika isipokuwa talaka? Bora nyie mabwana acheni maneno kama hayo bali jitengeni na *Neyoga*. Yafaa nini maneno kama haya kwamba katika *Neyoga* kuna manufaa mengi na siri nyingi? Enyi mabwana, kwa akali epukaneni na desturi hiyo hadi siku za kuondoka tauni, isije balaa hili likatapakaa zaidi kwa

matendo kama hayo. Ni masikitiko kwamba juu ya desturi hii ya *Neyoga* ambayo walipaswa kuionea haya, Waaria wamezidi katika midomo michafu. Baadhi ya Waaria waungwana waliohudhuria katika mkutano wa Qadian walinijia na wakakiri wenyewe kwamba katika mkutano maneno machafu sana yalisemwa, na hususan Waaria wengi wakamtaja mtu mmoja aliyekuwa mkali zaidi na mwenye midomo michafu sana.

Basi, ibainike kwamba dini haimaanishi kupinga hovyo pasipo kutafakari, na kufanya dhihaka kwa kuongeza shamrashamra za mkutano na kufanya mzaha kama waigaji, kwa njia hiyo dini yoyote haiwezi kuimarika. Kwa waja wema njia bora ndiyo wayapinge mafundisho yaliyokwisha tangazwa na dhehebu fulani, lakini wasikipinge kitabu cha kimbingu cha dini fulani maadamu hawajajua kikamilifu na kuelewa hoja zote kitimilifu. Kwa mfano, kuna suala la *Neyoga*. Hamna shaka kwamba juu ya mume kuwepo hai, mkewe kulalana na mtu mwingine, si mara moja tu bali hadi miaka kumi na miwili au kumi na mitatu mpaka watoto kumi na mmoja wazaliwe, ndio upujufu ambao dhamiri ya binadamu haiukubali na kila tabia njema inaukimbia kabisa.

Na kwa hakika hamna upujufu zaidi ya huo. Na hakuna mwenye staha atakayependa kumwona mkewe katika hali kama hizo ilhali yeye mwenyewe yuko hai. Lakini Jumuiya yetu iliyosimamishwa kwa ajili ya ucha Mungu izingatie vizuri kwamba hilo si fundisho la Veda. Rai yangu ndiyo hii hii kuwa hilo silo fundisho la Veda. Naelewa vizuri kwamba wakati mwingine *shurti* moja au aya yaweza kuwa na maana ishirini, basi hapo mtu mwovu anachukua maana ile iliyo mbaya, na mtu mwenye tabia njema huchukua maana nzuri. Wapo baadhi ya watu ambao kwa sababu zao za kinafsi hupenda kueneza maovu ndani ya kaumu. Basi, hao kwa kutafuta udhuru wanatoa *shurti* au aya fulani kutoka katika kitabu ambacho kinafahamika kuwa cha kimbingu na kwa njia hii wanawaangamiza majahili. Hivyo, Jumuiya yetu iepukane na njia kama hizo, kwani hizo ni kinyume cha tahadhari na unyofu. Mambo yale yanayopatikana katika karibu kaumu zote, kuyakinza ni ujahili moja kwa moja au ni chuki bila sababu wanayoonyesha Waaria. Kwa mfano kuoa wake zaidi ya mmoja, au kutaliki wakati wa haja na mengineyo yaliyopo katika kaumu zote kuyapinga si kazi ya mtu mwungwana, kwani hayo yanakuwepo ndani ya

kila kaumu. Kwa hakika yanayopaswa kupingwa ni mambo mawili. La kwanza, roho na miili havikutokana na Mungu, yaani havikuumbwa na Mungu, bali ndio miungu wenyewe wa kuwepo kwao, na vipo tangu azali kama Alivyo Mungu. Pili, njia hii ya ukaramshi iitwayo *Neyoga*. Na ukinzani huo sio dhidi ya Veda, bali wamhusu Pandit Dayanand aliyeeneza dhehebu kama hilo. Jumuiya yetu ijitahadhari, isipate kusema lolote pasipo sababu. Ni sawa kuwa kati ya Waaria wapo wengi wakali wasioangalia, pindi wakinzapo, kwamba wameisha chunguza kiasi gani kuhusu ukinzani huo, bali hutamka tu chochote bila kujali. Shabaha ndiyo kufanya masihara, siyo utafiti. Baadhi yao baada ya kusoma Kitabu cha Mungu kijuu-juu, tu haraka wanaanza kupinga pasipo kuzingatia kikamilifu. Katika Neno la Mungu mahala fulani pana istiara na mahala fulani pana majazi, na mahali fulani panakusudiwa kuonyesha uhakika. Basi, kama hamna ujuzi mkamilifu, na moyo pia sio safi, hapo kupinga huwa ujahili. Walifahamuo Neno la Mungu ndio wale waunganao na Mungu. Mtu yule aliyezama kikamilifu ndani ya uchafu wa dunia, macho yake yamepofuka na moyo umechafuka, atalipingaje Neno la Mungu! Yapasa

kwanza ajitakase moyo wake, ajitenge mbali na tamaa za nafsi, kisha alete upingamizi. Kwa mfano imeandikwa katika Kurani Tukufu:

وَمَنْ كَانَ فِيْ هٰذِهٖٓ اَعْمٰى فَهُوَ فِي الْاٰخِرَةِ اَعْمٰى[7]

yaani yule aliye kipofu hapa duniani, atakuwa kipofu huko Akhera pia. Sasa yule mkinzani asiyeelewa kusudio la Neno la Mungu atapinga akisema, angalieni, imeandikwa katika dini ya Islam kwamba vipofu hawatapata wokovu, maskini kipofu ana kosa gani? Lakini yule atakayeisoma Kurani Tukufu kwa makini kwa kujiondolea chuki, atafahamu kwamba hapo vipofu sio vipofu wa macho, bali vipofu wa nyoyo. Ndiyo kusema kwamba wasiomwona Mungu hapa duniani, hawatamwona huko akhera pia. Kadhalika kuna mamia ya majazi na istiara ndani ya Neno la Mungu, mwenye harara ya nafsi haraka sana atazipinga hizo zote. Nasema kwa kula kiapo kwamba ni kweli jambo hili kuwa kwa kulifahamu Neno la Mungu, kwanza yapasa kujitakasa moyo kutokana na harara ya nafsi, ndipo nuru ya Mungu itauteremkia kutoka kwa

---

[7] Banii Israaiil, 17:73 — Mwenezi

Mungu. Pasipo mwanga wa ndani, uhakika wenyewe hauonekani, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu:

لَّا يَمَسُّهُۥٓ إِلَّا ٱلْمُطَهَّرُونَ[8]

yaani, hili ni Neno Takatifu, maadamu mtu hatakasiki, hatazifikia siri zake. Nilikuwa kijana, sasa ni mzee, watu wakitaka waweza kutoa ushahidi kwamba sikushughulikia mambo ya dunia, na daima nilipenda shughuli za dini. Nimelikuta Neno hili liitwalo Kurani, limejaa hekima zilizo takatifu na za kiroho. Hilo halimfanyi mtu yeyote kuwa Mungu, wala halimlaumu Yeye kwa kuviondoa roho na miili katika uumbaji Wake. Na ile baraka ambayo kwa kuipata dini inakubaliwa, Neno Hilo hatimaye laiteremsha moyoni mwa mtu, na kumpatia fadhili za Mungu. Basi, kwa nini turudi gizani tukiishapata mwanga, na kwa nini tuwe vipofu tukiisha pata macho!

Hapa nimelazimika kuongeza kusema kwa sababu tu ya kuihami kweli — jambo lililo faradhi yangu — kwamba kwa kuacha mambo haya machache, wafuasi wa *Sanatan Dharm* ni afadhali mara elfu

[8] Al-Waaqi‘a, 56:80 — Mwenezi.

kuliko Wa-Aria Samaj hivi kwamba hawaiondolei heshima *Parmeshar* (Mungu) wao kwa kusema kuwa sisi tukiwa tangu azali na kwamba hatukuumbwa, basi tuko sawa Naye. Na hawalikubali suala la upwamu la *Neyoga*. Hawaipingi ovyo Islam, kwani wanajua kuwa mambo ya Islam yamo katika kaumu zote kwa usawa. Hao wengi wao hupenda urafiki, hawana ujeuri wala ukali sana. Na mbele yao, Waaria wasijisifu kwa kusema hatuabudu masanamu wala hatuwaamini Ma-Autar, kwani ma-jogi (watawa) wa Sanatan Dharm ambao wana daraja la juu la dini nao wanajitenga na ibada ya masanamu. Ama kuhusu Autar, basi ieleweke kuwa katika lugha ya Kisanskriti manabii na mitume huitwa Ma-Autar wanaoshukiwa nuru ya Mungu. Basi dini hasa ya Sanatan Dharm siyo kwamba Autar aabudiwe. Naam, wanawaheshimu na kuwa na mapenzi yao.[9] Lakini nimeona katika baadhi ya majarida na

---

[9] Kuwapenda wanadamu wema ndiyo faradhi ya wenye imani, na kwa njia hii sharti ya kukaa na watu wema yatimizwa. Na Wa-Sanatan Dharm si tu wana mapenzi ya Ma-Autar waliopita, bali wanangojea ujaji wa Autar wa mwisho katika zama hizi atakayetakasa ardhi akifutilia mbali dhambi. Basi, si ajabu, wakati fulani, wenye bahati njema miongoni mwao waipokee silsila hii ya kimbingu kwa kushuhudia ishara za Mungu, kwani hawa wana ukaidi kidogo sana — Mwandishi.

magazeti ya Aria Samaj kwamba baadhi ya wajeuri waliwadhihaki Ma-Autar na kusema maneno ya kukosa adabu. Hiyo siyo kazi ya watu wema. Ni hakika ya kuwa ujeuri wa baadhi ya Waaria umepita mipaka. Ujeuri huo unathibitisha kuwa huo ndio mmea usio na mzizi. Hao watu hawana maelekeo kwenye mambo ya roho. Huwezi kujipatia dini kwa ujeuri na ujanja, dini yataka mauti ambayo baada yake roho hai yatolewa. Ole wao, baadhi ya Waaria wenye tabia ya kibaruti wasiojua dini ni kitu gani wakaitukana Islam kama waigaji katika mkutano mjini Qadian.[10] Kama wangelikuwa na nia njema wangeliniandikia kuwa wanacho kipingamizi fulani dhidi ya Islam. Nami — ingawaje nilikuwa siwezi kuhudhuria katika vikao kama hivyo —

[10] Hao watu si tu walitumia midomo michafu dhidi ya Islam, bali pia walikosoa na kuaibisha sana mafundisho matakatifu ya Sanatan Dharm na kuwaudhi maskini Mabaniani nyoyo zao. Wakaishambulia vilevile dini ya Kikristo pasipo haki sawa na tabia yao. Kupita kiasi wakati wa kushambulia ndiyo tabia ya kishetani. Ni sawa kabisa kwamba Hadhrat Isa si Mungu, lakini alikuwa ni nabii mpendwa na mtume mpendwa wa Mungu. Na ni kweli kwamba Raja Ram Chandar na Raja Krishna hawakuwa miungu, lakini pasipo shaka wote hao wawili walikuwa waja wa Mungu na manabii. Ufunuo ung'aao wa Mungu uliwateremkia nao wakaitwa Ma-Autar (manabii) — Mwandishi.

ningeliwatuliza kwa kuondolea mbali wasiwasi wao kwa upole na maelezo bayana. Lakini sasa walivyokuja Qadian ndivyo walivyorudi wakijitwika rundo la ujeuri na matusi. Hata hivyo, kwa kuandika kitabu ‘Nasime Da‘wat’, nimewaalika tayari. Hata kama mmojawapo tu kati yao akijaaliwa kufahamu nitapata ujira.

## Tamati

Nimekwisha eleza katika kijitabu Nasime Da‘wat kwamba kila dini huchunguzwa kwa njia tatu. Kwanza, dini hiyo imeandika nini kumhusu Mungu. Nasikitika kwamba mafundisho ya Aria Samaj hayaoni kwamba Mungu ndiye chanzo cha vitu vyote vilivyopo, bali huamini kila kitu kipo tangu kale, kipo tangu azali, kipo chenyewe pasipo kuumbwa. Hao wanayo itikadi kuwa Mungu Hakuviumba vitu hivyo wala nguvu zao. Basi, ni wazi kwamba Mungu wa Aria Samaj si Mungu kwa hakika, waila ilipaswa vitu vyote vingetoka kwake. Imekuwaje Yeye aitwe Mungu, lakini vitu vingine viwepo vyenyewe! Kisichoumbwa naye kimekuwaje kuwa chake!! Mwaria yeyote atueleze sababu ya kutwaa huku kusiko halali. Vitu asivyoumba Mungu, ni dhuluma tu Yeye kuvitawala. Hivyo, kama Wa-

Aria Samaj wanawasuta Wa-Sanatan Dharm kwa sababu ya kuabudu masanamu, basi wao wenyewe wanasutwa zaidi kwa itikadi yao hiyo. Kwani waabudu masanamu hawaamini masanamu na *ma-Deyota* yao kwamba yapo yenyewe pasipo kuumbwa; wanaamini tu kwamba *ma-Deyota* na ma-Autar wamejaaliwa na Mungu nguvu kubwa kubwa ambazo kwa sababu ya hizo wanawatimizia watu haja zao.

Basi, inagawaje jambo hilo si sawa, bali atimizaye haja ni Mmoja tu, yaani Mungu anayeitwa *Parmeshar*, na mtu yule tu anapata heshima duniani na Akhera amtiiye Mungu akiachana na wote. Kila wakati sauti yasikika kutoka Kwake Yule Mtukufu, 'Kama ukiwa Wangu, ulimwengu mzima utakuwa wako.' Tumejaribia hilo hilo, nasi tu mashahidi wake. Yule mtu anayejisahau katika mapenzi Yake, na akiungua katika moto wa penzi Lake atajipatia uwepo mpya. Basi aingiapo ndani ya moto huo, hapo vitu vyote wa ardhi na mbingu waviabuduvyo watu wengine huwa watumishi na mahadimu wake. Ilmuradi, hili ni kosa la Wa-Sanatan Dharm kuwa wanaviomba vitu hivyo mahitaji yao, na hawajifaidishi kwa ile nuru hai ing'aayo iliyo mbele yao, na haiko mbali, bali i karibu zaidi kuliko mawe hayo wanayochonga.

Lakini, hata hivyo wanaamini kwamba kila kitu kimetokana na Mungu, pasipo Huyo hakuna kilichopo chenyewe. Yaonekana hayo ndiyo mafundisho ya Veda, ambayo Wa-Sanatan Dharm hawakuyasahau. Kwa kuona mambo ya wale *marishii* (manabii) na *ma-munii* (watawa) waliofanya mazoezi makubwa makubwa ya kiroho huko Bannu, twafikiria kwamba uhakika wa Veda uliwafunukia. Kwa hiyo, hao hawaamini kama Wa-Aria Samaj kwamba roho na chembe-chembe zipo tu zenyewe tangu azali, bali kama inavyodhihirika katika maandiko yao, itikadi yao ilikuwa hii tu kwamba kila kitu kimetokana na Mungu, yaani ndiyo matamshi yake. Hiyo ndiyo dini ya Kiislamu. (Wenye busara mia, akili yao moja; ujahili ndio wa kila mmoja). Hao watu hawakuitegemeza dini kwenye ujanja wa kutongoa, bali walimtafuta Mungu kwa mazoezi ya kiroho, bidii, auradi na ibada kwa moyo kabisa na wakienda huko Bannu wakajitahidi sana na kujibidiisha mno wakanyausha miili yao kwa kufunga saumu sana, na kuishi upwekeni wakiwa na mapenzi ya Mungu, ndipo ikawadhihirikia ile nuru ya kale inayoitwa kwa lugha mbalimbali *Parmeshar*, *God, Khudaa* na *Allah*. Hawakuwa na imani kwamba ufunuo na wahyi wa Mungu

uliishia kwa Veda na tangu hapo binadamu akafungiwa milango ya kuongelea na Mungu na kutiliwa kufuli. Bali, Mungu Alikuwa Anaongea nao, na habari za ghaibu zikawadhihirikia. Kweli yenyewe ni kwamba wamtafutao Mungu wanaojifia katika njia yake na wanaachana na vitu vyote kwa ajili yake, kama Mungu Asingewajali na Asingejidhihirisha kwao, na Angeendelea kujificha, hata na sauti yake isingesikika, hapo hao wangeangamia wakiwa hai, wala asingekuwa yeyote duniani mwenye bahati mbaya kama hao, kwani wakatengana na dunia kwa ajili ya Mungu, lakini hawakumpata; wakakosa zote mbili, dunia na pia akhera. Lakini, je rafiki mmoja anaweza kumtendea hivyo rafiki yake. Hata kidogo. Kuna methali mashuhuri kwamba katika urafiki, wawili wawe waaminifu. Mmoja wao ananasika katika huba ya mtu na kwa muda fulani anamvutia mpendwa wake ndani kwa ndani usiku na mchana kwa uchungu na kuudhika, ndipo mara mwako wa huba — sharti huba hiyo siyo kwa tamaa mbaya — wamwangukia mpendwa huyo moyoni mwake ambaye alikuwa hajajua, ndipo yule mpendwa pia anapata hisa katika uchungu wake, kana kwamba uchungu wake na vite vyake vyamwathiri mpendwa, hapo moyo wake huvutika kwake, na

pasipo sababu zijulikanazo yaingia moyoni mwake kwamba mtu yule ananipenda, tena siyo kutiliwa moyoni tu, bali hatimaye huyo ananasika katika mapenzi yake, na moyo huunganika na moyo, kana kwamba hao wawili wanakuwa mmoja. Na ni la ajabu sana kwamba mpenzi akiyaficha mapenzi yake hata namna gani, mpendwa wake hakosi kuyatambua. Kisha dunia pia ambayo humchunguza kila mtu kama jasusi, yatambua kwamba hao wawili wanapendana. Kisha mapenzi hayo — kama kweli ni mapenzi safi yasiyo na ubaya wa tamaa mbaya ndani yake — yataka kuwafikia hao wawili hata kwamba nyoyo zao huvutana. Hawapati utulivu pasipo kuona, nao hawatambui huo mvutano umetokea wapi na umezalikaje! Hatimaye nyoyo zao safi hupenda kupata ladha ya kuongea kidogo na kuonana mara moja. Mioyo yao huhangaikia kusikia neno moja, hata kama wajifie baadaye. Hivyo, huu ndio mwisho wa mapenzi ya kidunia kwamba upeo wake ni kuongea pamoja. Basi, ilaaniwe ile dini isiyomwahidi mpenzi wa *Parmeshar* hata kiasi hiki kwamba Yeye Atasema naye jinsi mpenzi wa mtu anavyosema na mpendwa wake. Ole wao, hata hawanayo imani kama hiyo watu hao. Lakini hatuwezi kukubali

kuwa Veda yataka kumnyima mtu daraja hii ya maongezi, bali hayo ni makosa ya watu hao, siyo taksiri ya Veda. Mimi nasema kweli kabisa kuwa dini ndiyo ile tu inayomwunganisha mtu na Mungu na kumwonjesha ladha ya maongezi yake. La sivyo, ni kuingiza tu mkono ndani ya kinyesi ambamo hamna kitu isipokuwa uchafu.

Njia ya pili kuchunguza dini ni kwamba dini ya kweli huunganisha na Mungu, na kadhalika hueneza usafi katika kaumu.Tumekwisha andika kwamba Aria Samaj haimwunganishi mtu na Mungu, bali huukana hata ule mwungano wa asili uliopo wa kila roho kwa *Parmeshar* kwa sababu ya hiyo kuwa kiumbe; na mfano wa usafi ni dhahiri kutoka katika mafundisho ya *Neyoga*. Shabash! Ewe Sanatan Dharm, kwani hukuifahamu kila chembe na kila roho kuwa *Parmeshar* wa uwepo wake, wala hukuingiza uchafu wa *Neyoga* katika itikadi yako. Nasema kweli kabisa kwamba kama ukikanyaga hatua mbele kiasi cha kuwa kama *majogi* (watawa) mawalii wanaojaa mapenzi ya *Parmeshar,* na kumkurubia Yeye hata kwamba uitupilie mbali ibada ya masanamu, ndipo ushindi ni wako katika kila medani dhidi ya Waaria. Hao watakuja kwa njia moja kukabiliana nawe, na watakukimbia

kwa njia saba. Na hili si jambo jipya; tangu kale *majogi* wanaojiunguza katika moto wa mapenzi, dini yao ndiyo hii hii kwamba minghairi ya *Parmeshar* kila kitu si chochote wala lolote.

Njia ya tatu ya kuichunguza dini ya kweli ni kwamba dini hiyo inamwondolea mtu kiasi gani taka za dunia na kumfikisha kwa Mungu kumwonyesha Yule Mtakatifu. Dini ya Aria imenyimwa kabisa daraja hiyo. Hao hadhi yao siyo isipokuwa matusi na midomo michafu na dharau. Mafundisho yao yenyewe siyo nadhifu kuhusiana na *Parmeshar*, wala siyo safi kuhusu utakaso wa kaumu. Wala hawana hadhi katika baraka zile wanazojaaliwa waja wa Mungu. Nimewahi kusikia kwamba Wa-Sanatan Dharm wa Qadian wananuia kufanya mkutano kwa kupinga na kubatilisha mafundisho mawili waliyo nayo Wa-Aria Samaj kuhusiana na ukalili wa uwezo wa *Parmeshar* na kuhusu *Neyoga*. Rai yangu ni kwamba Wa-Sanatan Dharm wa miji mwingine wapaswa kuwasaidia; tukiona hali mwafaka nasi pia tutashiriki kuwasaidia.

**Wassalamu**
**Mnyenyekevu Mirza Ghulam Ahmad**
**Wa Qadian**